

MSIKIENI YEYE



Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu wa maombi.

² Baba wa Mbinguni mwenye rehema, usiku wa leo, tunapokuja tena, tukija katika Uwepo Wako wa Kiungu tukiomba rehema, tunashukuru kwa yote ambayo umetufanyia katika siku zilizopita. Tunaomba ya kwamba Wewe utakuwa pamoja nasi tena usiku wa leo, na utuonyeshe tu Uwepo Wako tena usiku wa leo.

³ Tunakushukuru kwa ajili ya watu wote ambao wamemjia Kristo kwenye wakati wa uamsho huu, na kwa ushirikiano mzuri wa wahudumu na watu wote, na wema wao.

⁴ Tunakushukuru kwa ajili ya uponyaji wote ambao umefanya na kutenda, barua zinazoingia, na watu wakishuhudia wakati walipoenda nyumbani na kivimbe kikaanguka kikawatoka, wapendwa waliponywa kwa kuwekewa lesa, na wengi, angalau wawili au watatu tunaowajua tayari wameshuhudia ya kwamba walikuwa kwenye viti vya magurudumu na wakaenda nyumbani halafu kesho yake asubuhi, mbona, wakaanza kujisikia vizuri zaidi, na siku moja ama mbili walikuwa wametoka na kwenda zao.

⁵ Mungu, jalia kwamba kila mmoja ataponywa, Bwana, ingawa huenda tukawa mbali sana nchini litakapotukia, lakini Wewe pokea utukufu, Bwana. Na ambapo itakuwa tu ni ushuhuda katika ujirani na miongoni mwa watu kwa ajili ya wema na rehema Zako.

⁶ Hapa usiku wa leo kuna vitambaa vingi na lesa zimewekwa hapa kwa ajili ya wagonjwa na wanaoteseke. Mwenyezi na Baba wa Thamani, jalia Roho Mtakatifu awafunike hawa sasa katika tendo hili la imani, jalia yeyote zitakazowekwa juu yake, jalia waponywe, Baba. Wewe ni Mungu, jalia rehema Zako za Kiungu zikae juu ya watu wanaovaa hizi, na jalia kusiwe na m—mmoja ila ambaye ataponywa.

⁷ Nena nasi usiku wa leo kupitia Neno Lako, nena nasi kupitia Roho, nasi tutakapoenda nyumbani usiku wa leo, na tuseme kama wale waliokuwa wakitoka Emau, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?” Kwa kuwa tunaomba, katika Jina Lake, na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

⁸ Mwaweza kuketi. Je, ni sawa huko juu kwenye roshani sasa, mnaweza kusikia vizuri huko juu upande *huu*? Upande *huu*? Sawa, hilo ni zuri.

⁹ Nilikutana na baadhi ya marafiki mlangoni pale, nao walikuwa wamechelewa kidogo wala wasingeweza kupata ninii, hapa chini kwenye sakafu hii, kwa hiyo nikawaambia sikujua kama walikuwa wakisikia vizuri sana kule juu, lakini nina furaha ni sawa sasa.

¹⁰ Kesho alasiri ni, inasikitisha kusema, lakini ni kumalizia kwa uamsho huu. Hakika umekuwa wakati mzuri sana kwetu. Nasi tunathamini kila kitu, wema, na yote ambayo yamefanywa. Tunawashukuru kwa moyo wetu wote, na kutumaini ya kwamba mtakuwa pamoja nasi kesho alasiri.

¹¹ Sasa, kuna—kuna wageni hapa kutoka miji mingine, moteli ninayokaa imejaa kabisa, na, kutoka kwenye moteli zingine. Na wakati mkiwa hapa, sasa, asubuhi, kutakuwa na shule ya Jumapili kwenye makanisa haya hapa, na, makanisa haya ya Full Gospel hapa bondeni, na bila shaka watawakaribisha kwenye yoyote ya ibada zao, nadhani tayari imetangazwa mahali watu walipo, na kuja kuwasikiliza watu hawa. Sasa, mnakuja kusikia huduma ya namna hii, watu hawa wanakuja hapa kuiwakilisha, nao wanahubiri na wana mambo yale yale tunayotetea hapa, watawafaidi. Waleteni watoto wenu kwenye shule ya Jumapili, mkawaweke katika shule ya Jumapili.

¹² Unajua, ni dhambi kuwatumia watoto wako kwenye shule ya Jumapili, mnajua hilo. Ambataneni nao. Msiwatume, nendeni pamoja nao. Ni dhambi kuwatumia, nanyi mnakaa nyumbani, kwa hiyo ne—nendeni tu pamoja nao. Waleteni kwenye shule ya Jumapili, nanyi mtayapata madarasa, na waalimu, na kadhalika.

¹³ Halafu tutakuwa na ibada yetu ya Jumapili—ibada yetu ya Jumapili alasiri, kwa sababu basi makanisa yanaendelea na yanaweza kuwa na ibada ya Jumapili usiku. Na wote ambao wameongoka katika mikutano hii, katika wakati huu hapa, tumefanya miito ya madhabahuni...

¹⁴ Nanyi mnaona siku hizi, dhambi ni nzito sana, hata wenye dhambi hawavutiwi zaidi sana na Kristo. Mnajua, ninaamini Yeye karibu ameacha kuwaita. Mnajua kutakuwa na wakati ambapo mwenye dhambi wa mwisho atamjia Kristo, wala hakutakuwako na zaidi, mnajua hilo. Mwili wa Kristo hautakuwa mwili dubwana, hautakuwa na kidole kimoja cha ziada, kwa sababu ya wewe au mimi. Huo Mwili utakapokamilika, kazi imekwisha, Mungu atairudisha Roho Yake kwa Wayahudi, nao Mataifa wataingia katika Unyakuo. Sasa, kwa hiyo tunataka kuwa na hakika ya kwamba kila mtu...

¹⁵ Na wakati mwingine labda hapa Marekani, nilikuwa nikiwazia leo nilipokuwa katika maombi, jinsi ambavyo uamsho wa siku kumi, na waongofu wachache tu. Nikawaza, “Nchi za ng’ambo, uamsho wa siku kumi labda ungeleta laki mbili, ama labda waongofu nusu milioni katika mkutano wa siku

kumi huko Afrika, ama mahali fulani namna hiyo.” Lakini mnajua inatubidi kumkamata kila mmoja? Mnaona, nafsi moja ina thamani ya dunia elfu kumi.

¹⁶ Siku moja, nilikuwa nimesimama karibu, katika u—ukumbi mduara wa michezo, nami nilikuwa nikitazama na kuangalia kila mahali, nikiangalia sanaa na maonyesho, ndipo nikaona uchanganuzi wa mwili wa mwanadamu. Basi kulikuwako na vijana wawili, wamesimama wakiangalia huu, nao ulisema ya kwamba mtu aliyekuwa na uzito wa ratili mia moja na hamsini, alikuwa na thamani ya senti themanini na nne katika kemikali. Alikuwa tu na karibu chokaa ya kutosha ndani yake kunyunyizia kiota cha kuku, na—na *kiasi tu* hata kemikali hizo zilikuwa na thamani ya senti themanini na nne.

Mmoja wa hao wavulana aliangalia huo na kusema, “Vema, Jim, sisi hatuna thamani kubwa sana sivyo?”

¹⁷ Nikawazia, “Hiyo ni kweli, mwili huu hauna thamani kubwa, lakini hata hivyo tutaweka ko—kofia ya dola kumi juu yake, koti la cheche la dola hamsini, tunainua pua yetu, kama ingenyesha, ingetuzamisha.” Mnaona? Tunafikiri sisi ni watu mashuhuri, tunajivika nguo kabisa, na kujipamba vizuri, kisha tunaenda zetu, tunashughulikia hizo senti themanini na nne.

¹⁸ Unaingia kwenye mkahawa, nao wakikupa bakuli la supu na lilikuwa na buibui ndani yake, ungeushtaki huo mkahawa, unazichunga hizi senti themanini na nne. Lakini una nafsi humo ndani ambayo ina thamani ya ulimwengu elfu kumi, nawe utasukumiza chochote ndani yake, ulimwengu, tamaa mbaya, chochote kile, na ni—ni ya Milele na ina thamani ya ulimwengu elfu kumi. Lakini tunaangalia hizo senti themanini na nne, na kuachana na ile ya thamani ya ulimwengu elfu kumi. Hilo si ni jambo fulani?

¹⁹ Nilimshika mvulana huyo kwenye bega, nikasema, “Hiyo ni kweli mwanangu, hatuna nyingi sana katika mwili huu, ni kemikali chache tu, bali nafsi iliyo ndani yake ilimgharimu Mungu Mwanawe.” Hiyo ni kweli.

²⁰ Maskini ombaomba mmoja, si muda mrefu uliopita, huko Louisville, Kentucky, naamini ndiko, ambaye alikuwa akisambaza vitini mtaani, ndipo motokaa ikamgonga, na karibu ivunje kila mfupa ndani yake. Wakamkimbiza, hospitali ya mjini, na—naye alikuwa na hali mbaya sana hata wao—wao wakawazia hakukuwa na haja ya kujipumbaza na huyo mzee.

²¹ Kwa hiyo, madaktari wakafanya ushauri kidogo, na kusema, “Yeye si, ana hali mbaya sana, yeye, na ni mzee, ha—haustahili.” Kwa hiyo, walidhani huyo mzee alikuwa, asingeweza kuwasikia, bali hakuwa—hakuwa amekufa kama walivyodhanika. Kwa hiyo wakati wao. . . Dakika chache kwa nini ninii, wakasema, “Vema, hebu tumrudishe tu chumbani mwake.”

²² Ndipo huyo mzee akageuza kichwa chake, na kusema, “Naam, nina thamani fulani, pia.” Akasema, “Nina thamani kubwa sana hata Mungu akamtoa Mwanawe wa pekee ili niwe na Uzima wa Milele, nami niliukubali huo miaka hamsini iliyopita, nami nimesimama mitaani nikisambaza vitini tangu wakati huo.” Naye akasema, “Leo Yeye ni mtamu zaidi kwangu kuliko alivyowahi kuwa hapo awali.” Hiyo ni kweli. Tunaweka thamani mahali pasipofaa. Mnaona? Wakati mwingine, tunaangalia mambo...

²³ Mnajua, wakati Yohana Mbatizaji alipokuja akihubiri katika nyika ya Uyahudi, manabii wote walikuwa wameshuhudia juu ya wakati huo, kasema, “Mahali palipoinuka patashushwa, mi—milima itaruka kama kondoo dume wadogo, na majani yote yangepiga makofi yao, na ni tukio kuu jinsi gani!”

²⁴ Basi ilitukiaje? Watu, watu wa kidini wa siku hiyo, walidhani ya kwamba Kristo angeshuka kwa gari la farasi kutoka Mbinguni, na—na fimbo ya chuma, bali wakati Yeye alipokuja, aliyekuwa akiuleta huo Ujumbe wa mwisho alikuwa ni maskini mhubiri mmoja, nusu uchi, huku amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo, masharubu usoni mwake kama mdudu aliyejaa manyoya, na huyu hapa Yesu anakuja, Mtu wa kawaida tu, akitembea, naye akabatizwa majini, kwenye maskini ukingo wa Yordani uliojaa matope. Lakini mnaona, katika, kile mwanadamu anachoita kikuu, Mungu anakiita upumbavu; kile mwanadamu anachoita upumbavu, Mungu anakiita kikuu. Kwa hiyo akili ya mwanadamu tu ndiyo imepotoshwa, mnaona, na kinyume chake tu.

²⁵ Sasa, ninyi ambao mmekuwa mkiandika muhtasari, na halafu kabla hatujasoma Maandiko, mnaweza kufungua Injili ya Mathayo Mtakatifu, mlango wa 17, nasi tuta—tutasoma.

²⁶ Na wakati tunaposoma ningetaka kusema ya kwamba kesho alasiri zile kadi za maombi, tutajaribu kugawa kadi zote za maombi ambapo tunaweza kugawa kesho alasiri, na kujaribu kumleta kila mtu anayetaka kupitia kwenye mstari wa maombi, kuwapitisha. Hatuwezi, hatuwezi kufanya upambanuzi wote, lakini tunaweza, angalau kuwawekea watu mikono na kuwaombea. Kwa hiyo, njoni kesho alasiri kwa ajili ya ibada. Hiyo itakuwa ndiyo ibada yetu ya mwisho katika uamsho huu, na labda, ya mwisho kati ya namna hizi za ibada utakayowahi kuona maishani mwako, huduma inabadilika kuwa kitu ambacho kitakuwa kikuu zaidi.

²⁷ Mlango wa 17 wa Mathayo Mtakatifu:

...baada ya siku sita Yesu akawatwaa Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye, akawaleta juu ya mlima mrefu faraghani,

Akageuka sura yake mbele yao: uso wake ukang'aa kama jua, na mavazi yake yakawa meupe kama nuru.

Na tazama, wakatokewa na Musa na Eliya wakizungumza naye.

Petro akajibu, akamwambia Yesu, Bwana, ni vizuri sisi kuwapo hapa: ukipenda, na tukufanyie Wewe vibanda vitatu. . . tufanye hapa vibanda vitatu; kimoja chako weve, . . . kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya.

Alipokuwa katika kusema, tazama, wingu jeupe likawatia uvuli: na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependeza naye; msikieni yeye.

Na wale wanafunzi waliposikia, walianguka kifudifudi, wakaogopa sana.

Yesu akaja, akawagusa, akasema, Inukeni, . . . msiohope.

28 Kama inampendeza Bwana wetu usiku wa leo kutoa kutoka kwenye fungu hili muktadha, ningetaka kuchukua somo la hayo Maneno matatu ya mwisho ya *Msikieni Yeye*. [Kiingereza: *Hear Ye Him—Mfa.*]

29 Ni kifungu kidogo sana. Mtu fulani huenda akasema, ukiwa na kusanyiko la ukubwa huu, “Mhubiri, ninaamini unapaswa kuwa na somo refu zaidi.”

30 Vema, labda hiyo ingekuwa hivyo, lakini kama kusanyiko hili litachukua tu somo hili, hilo tu ndilo tunalohitaji. Sio wingi, ni ubora. Ni kile lilicho. Ni Neno la Mungu, na kama tu utamsikia Yeye, kila kitu kitakuwa sawa.

31 Wakati fulani uliopita, ng'ambo ya mto kutoka mahali ninapoishi kulikuwa na m—mvulana mdogo aliyekuwa akizunguka kwenye dari kuukuu, naye alikuwa ameingia kwenye kasha la kale, naye akapata stempu ndogo ya manjano ya posta, naye akakumbuka ya kwamba huko chini mtaani kutoka kwake kulikuwa na mkusanya stempu, naye huyu mkusanyaji alinunua stempu za kale, ambayo ni kazi ya kujifurahisha; mimi huzileta kutoka Ulaya, Asia, na kila mahali kwa ajili ya wakusanya stempu hapa.

32 Basi mvulana huyu mdogo aliona stempu hii, na muda si muda mwajua, aliwazia, “Hii haina budi kuwa na thamani fulani, kwa sababu ni ya kale.” Kwa hiyo akifikiria koni ya aiskrimu akilini, aliwazia, “Nitaipeleka kwa mkusanyaji, na huenda, labda, nitapata za kutosha kupata koni ya aiskrimu.”

33 Ndipo akashuka mbio barabarani kwa mkusanyaji, akasema, “Bwana, nimepata stempu, na laiti ungeiangalia na kuona kama ina—kama ina thamani yoyote.”

Ndipo huyo mtu akachukua darubini yake, na chati yake, akasema, “Naam, ni stempu ya thamani. Unataka ngapi kwake?”

Akasema, “Vema, utanipa kiasi gani kwake?”

Akasema, “Nitakupa dola moja.”

Loo, ikauzwa *sasa hivi*, hiyo ilimaanisha kama koni kumi za aiskrimu. Kawazia, “Hiyo ni sawa.”

³⁴ Sasa, huenda nikakosea kwenye tarakimu zangu, kama nimekosea, na mtu fulani ameisoma, samahani. Lakini nafikiri huyo mkusanyaji aliua stempu hiyo yapata majuma mawili baadaye, kwa dola mia tano, halafu basi ikauzwa tena kwa dola elfu moja mia tano. Nami ninasahau sasa hiyo stempu imeleta kiasi gani, mahali ilipo sasa, iko *mbali* kwenye mamia ya dola.

³⁵ Sasa, haikuwa thamani ya kipande hicho kidogo cha karatasi ya manjano, ilikuwa ni kile kilichoandikwa kwenye karatasi hiyo, hiyo, thamani yake. Haikuwa ukubwa wake, wala karatasi iliyokuwamo, ni kile kilichokuwa *kwenye* hiyo karatasi.

³⁶ Hivyo ndivyo ilivyo na somo langu usiku wa leo, si ukubwa wake, wala si karatasi ya Kihindi iliyoandikiwa ambayo inaipa thamani, ni Kile lilicho, ni Neno la Mungu, *Msikieni Yeye*.

³⁷ Wakati mwingine ni mambo madogo ambayo tu—tunaacha bila kufanywa ndiyo yanamaanisha mengi sana kwetu. Ninaamini imeandikwa mahali fulani katika Maandiko kwamba si mambo makubwa tunayofanya, kitu fulani, “Vema . . .” lakini mambo madogo tunayoacha bila kutekeleza, ama, methali, hiyo ni kweli.

³⁸ Haidhuru, wakati mwingine watu, kama vile wachungaji, mwinjilisti huja mjini, na—na labda huenda, kama Ndugu Oral Roberts, ama baadhi ya hao wainjilisti mashuhuri, ambao wana milango ya kila namna ambayo huwavutia makumi ya maelfu ya watu mkutanoni, na halafu wakiondoka watu watamdharau, labda, mchungaji, na kusema, “Vema, mtu huyo mashuhuri pamoja na mchungaji wetu . . .”

³⁹ Lakini kumbukeni, mchungaji wenu, yeye anachukuliwa tu katika Ufalme wa Mungu kama mwinjilisti yeyote, ama mtu mwingine yeyote, yeye anashikilia jukumu lake.

⁴⁰ Si muda mrefu uliopita, huko Canada, wakati hayati Mfalme George alipotembelea Vancouver nilikuwa pamoja na Ndugu Baxter wakati huo, naye Ndugu Baxter alikuwa akiniambia kuhusu Mfalme akipitia mtaani. Na loo, kama ulipata kumwona, alikuwa ni mtu hodari. Siku hiyo alikuwa anaugua sana, ilikuwa ni kabla ya kuponywa kwake ugonjwa huo wa kukacha kwa tishu za mwili, halafu alikuwa na ugonjwa wa tumbo, pia. Na kwenye gari, walisema alikuwa akiteseka sana, lakini kamwe usingejua, ameketi wima, akizungumza na raia wake alipokuwa akipita.

⁴¹ Bw. Baxter alisimama huko nyuma mahali fulani na kulia sana alivyoweza kulia, ndipo akasema, “Ndugu Branham, sababu ya mimi kulia,” akasema, “mfalme wetu alikuwa akipita.”

⁴² Ndipo nikawazia, “Huenda hilo likawa ni kweli,” naye malkia ameketi amevaa nguo yake nzuri, ya samawati, jinsi ambavyo hao watu waliokuwa raia wao walilia, kwa sababu kwamba walikuwa wakipita. Nikawazia, “Kama ingemfanya Mkanada alie kwa furaha, wakati mfalme alipopita, itakuwaje wakati Yesu atakapokuja, Mfalme wa Mbingu na nchi?”

⁴³ Wakazifungulia shule zote siku hiyo, na wakampa kila mmoja wao, hao watoto wadogo, bendera ya Uingereza kumpeperushia mfalme kuonyesha uaminifu wao. Ndipo mfalme alipopita, vema, watoto wote wadogo katika shule fulani walirudi ila msichana mmoja mdogo. Nao walishangaa kilichompata huyo mtoto mdogo, alikuwa ni jamaa mdogo tu.

⁴⁴ Ndipo mwalimu, wakati alipoita orodha, mtoto huyo hakuwepo. Kwa mshangao mkubwa, akakimbia mitaani, akiangalia kila mahali. Na akiwa peke yake, amesimama nyuma ya nguzo ya simu, huku ameinua maskini mikono yake, akilia kwa maskini moyo wake wote. Na kwa hiyo mwalimu akamkimbilia, na kusema, “Mpenzi, kuna nini? Je, hukupata kumwona mfalme?”

Akasema, “Naam, nilimwona.”

Akasema, “Basi, ulimpeperushia bendera yako?”

Akasema, “Naam, nilimpeperushia bendera yangu.”

Akasema, “Basi, kwa nini unalia?”

Akasema, “Nilimwona mfalme, lakini mimi ni mdogo sana mfalme hakuniona.” Nalo lilikuwa likiuvunja maskini moyo wake.

⁴⁵ Lakini hivyo sivyo ilivyo kwa Yesu, haidhuru wewe ni mdogo jinsi gani, ama unafanya kidogo jinsi gani, Yeye huandika kila kitu unachofanya, anajua yote kukuhusu, kama wewe ni mkubwa au kama wewe ni mdogo. Anajua yote kulihusu, nayo yote yameandikwa kwenye vitabu Vyake. Na wakati mwingine ni mambo madogo madogo ndiyo hutuinua kwenye mambo makubwa. Hatuna budi kuufanya Mwili wote wa Kristo ufanye kazi pamoja.

⁴⁶ “Msikieni Yeye,” hilo ni Neno la wokovu kwa kila mtu atakayeliadini; ambalo litampitisha mwenye dhambi kutoka mautini kuingia Uzimani, kama ataliadini, ambalo litamchukua—ambalo litamchukua mtu anayemtafuta Roho Mtakatifu, na kumpa Roho Mtakatifu, ambalo litamchukua mgonjwa aliyejawa na kansa, ambaye madaktari wetu wapendwa wamemkataa, wanasema hana budi kufa, litamwinua tena kuwa mwanamume mkamilifu, wa kawaida, mwenye afya

tena, ama mwanamke, litayafungua macho yaliyopofuka, ambayo hayajawahi kuona mwanga wa mchana, litafungua masikio ya viziwi, litakomboa kutoka kwenye hospitali ya wendawazimu. Loo, lina nguvu zote, kama utalipokea kama Neno la Mungu.

⁴⁷ Hapa, wakati wa yale mapinduzi ilisemekana kwamba mtu fulani katika je—jeshi alifanya uhalifu, hatia ya shirikisho, naye akashtakiwa katika mahakama ya jeshi, na akapatikana na hatia ya kutoroka wakati wa vita, na ma—mashtaka yalikuwa kwamba inambidi kupigwa risasi na kikosi cha kufyatua risasi.

⁴⁸ Naye alikuwa gerezani, ndipo siku yake ya kuuawa na kikosi cha kufyatua risasi ikaamuliwa. Rafiki yake mwema akasema, “Nitaenda, nami nitaenda kwa afisa wa cheo cha juu zaidi aliyeko.” Ambaye katika wakati huo alikuwa Rais wetu mpendwa Abraham Lincoln, Mkristo mashuhuri, Mmarekani mashuhuri.

⁴⁹ Na kwa hiyo mtu huyo akakutana na Bw. Lincoln akishuka kutoka kwenye gari, naye akasema, “Bwana, najua ya kuwa wewe ni mtu mwenye haki, mcha Mungu, nawe hungeutoa uhai wa mtu, lakini hata hivyo, mtu fulani amepatikana na hatia ya—ya kukimbia, kukwepa wajibu wake, ama mahali pake wakati wa vita, naye amepatikana na hatia, na hana budi kufa. Bwana, neno moja tu kutoka kwako litamsamehe huyo mtu.” Kasema, “Hivi hutamsamehe tafadhali, bwana?” Ndipo akapiga magoti, akasema, “Mtu huyo ana wasiwasi, naye aliingia woga, nami nimemjua tangu alipokuwa mvulana mdogo,” kisha kasema, “kwa kweli ha—hakukusudia kufanya hivyo, bali alishikwa na wasiwasi, huku bunduki, na mizinga ikifyatuka, akakimbia.”

⁵⁰ Bw. Lincoln, katika njia yake ya uungwana na ya Kikristo, alichukua kipande cha karatasi na kuandika pale, “Namsamehe mtu huyu. Abraham Lincoln.” Akasaini jina lake.

⁵¹ Huyo mtu akamshukuru Bw. Lincoln sana, akakinyakua kile kipande cha karatasi, akakimbia gerezani mbio alivyoweza. Akiwa raia, hakuruhusiwa, bila shaka, kuingia, ila tu kwa ombi, basi akampelekea mtu huyo hicho kipande cha karatasi, akasema, akamwita kwa jina, akasema, “Rafiki yangu, umesamehewa!”

Akasema, “Ninajua je kwamba nimesamehewa?”

Kasema, “Hiki *hapa* kipande cha karatasi kilichoandikwa jina la Bw. Lincoln, ‘Namsamehe mtu huyu, Abraham Lincoln.’”

⁵² Huyo Mtu akakichomeka kwenye seli, na kusema, “Usinijaribu. Kwa nini ufanye maisha yawe mabaya zaidi kwangu? Kwa kuwa wakati wangu ni kufa asubuhi, halafu hapa unakuja kunidhihaki kwa maskini ki—kipande kidogo cha karatasi namna hiyo? Kama Abraham Lincoln angalinisamehe, kingekuwa na mu—muhuri wa Marekani, na, loo, kungekuwa na sherehe kubwa kuihusu.”

⁵³ Akasema, “Bwana, hiyo ni sahihi ya Abraham Lincoln.” Ni kama tu *Hili* lilivyo Neno la Mwenyezi Mungu. Akasema, “Wewe wape watekelezaji *hiki*, nao watalitambua jina la Bw. Lincoln, nawe umesamehewa.”

⁵⁴ Akasema, “Toka kwenye hiki kizimba, sitaki kusikia tena!” Basi mtu huyo akakataa kukipokea, ndipo kesho yake asubuhi akauawa na kikosi cha kufyatua risasi, akafa kwa kuuawa hadharani. Halafu basi, hiki hapa kipande cha karatasi kilichoandikwa na kutiwa sahihi na Rais ya kwamba mtu huyo amesamehewa, siku moja kabla hajafa, nao wakampiga risasi, hata hivyo.

⁵⁵ Kwa hiyo basi kesi ilisikilizwa katika mahakama ya shirikisho, basi huu hapa uamuzi wa mahakama ya shirikisho la Marekani hii tunayoipenda: ulisema, “Msamaha si msamaha, isipokuwa upokelewe kama msamaha.”

⁵⁶ Hivyo ndivyo Maandiko haya yalivyo usiku wa leo, ni msamaha kwa kila mtu atakayeyapokea kama msamaha, ni uponyaji kwa kila mtu atakayeyapokea kama uponyaji, ni neema kwa kila mtu atakayeyapokea kama neema. Na chochote Mungu alichohadi, ni chako kama utakipokea kama Neno la Mungu. Lakini kama ni kipande kingine tu cha maandishi, hakina maana kwako. Lakini kama unaweza kukikumbatia na kusema, “Ni Neno la Mungu,” basi lina maana *fulani* kwako.

⁵⁷ Sasa, Yesu, ninii... Nimekuwa na majaliwa maishani mwangu ya kukutana na watu wakuu. Na ni jambo la ajabu kuona jinsi mambo yanavyoweza kuwa kinyume. Nimekutana na watu *waliokuwa* watu wakuu, halafu nimekutana na watu *waliodhani* walikuwa ni watu wakuu. Na hakika kuna tofauti nyingi sana kati yao. Mtu mkuu daima hatakuwa na maringo, bali atajaribu kukufanya ufikirie ya kwamba wewe ndiwe mtu mkuu na yeye si kitu; na mtu ambaye si kitu na anajaribu kuwa mkuu, ni vinginevyo tu.

⁵⁸ Na hiyo ndiyo sababu ninajua ya kwamba Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu. Alikuwa duniani bila hata ya kuwa na mahali pa kuzaliwa, ilimbidi kuazima tumbo la uzazi, ilimbidi kuazima hori. Ilimbidi kuninii... Aliingia kupitia tumbo la uzazi la kuazima, kisha akaondoka kupitia kaburi la kuazima. “Mbweha wana matundu, na ndege wa angani wana viota, lakini Mwana wa Adamu hana mahali pa kulaza kichwa Chake,” hata hivyo, ni Mfalme wa Utukufu, Mungu wa Mbinguni aliyefanyika mwili akakaa kwetu, hilo ndilo lililomfanya kuwa mkubwa, hilo ndilo lililomfanya kile alichokuwa, kwa unyenyekevu Wake.

⁵⁹ Unyenyekevu, njia ya kushuka sikuzote, ndiyo njia ya kupanda juu. “Yeye atakayejidhili, Mungu atamkweza; ajikwezaye atadhiliwa.” Njia ya kushuka ndiyo njia ya kupanda juu kwa mwaminio, kujinyenyekeza mbele za Mungu.

⁶⁰ Yesu alikutana na watu wa matabaka yote ya maisha, alikutana katika makundi makubwa, wakati mmoja alikuwa pamoja na maelfu, mia tano kwa wakati mmoja, kumi na wawili kwa wakati mmoja, watatu kwa wakati mmoja, na hata atakuja kwa mmoja. Hilo linamfanya kuwa mkuu, kwa sababu hakuna hata mtu mmoja anayeweza kumwita Yeye pasipo Yeye kuja papo hapo karibu nao. Hilo ndilo linalomfanya kuwa Mungu kwa sababu ya unyenyekevu Wake.

⁶¹ Na, mwajua, kila wakati kunapotokea tukio kuu... Hili tunalosoma habari zake, lilikuwa ni tukio kuu. Petro baadaye aliuita mlima mtakatifu katika moja ya nyaraka zake. Siamini ya kwamba Mtakatifu Petro alimaanisha kwamba mlima ulikuwa mtakatifu, si mlima mtakatifu, ni Mungu Mtakatifu juu ya mlima.

⁶² Si kanisa takatifu, ama watu watakatifu, ni Roho Mtakatifu kanisani na ndani ya watu. Si kanisa lililo takatifu, wala watu, ni Roho Mtakatifu aliye kanisani, huyo ndiye anayelifanya takatifu. Ninafurahia jambo hilo. Mungu ni Roho Mtakatifu, na Yeye Ndiye aliye mtakatifu. Naye, Uwepo Wake unaleta Uwepo Wake Mtakatifu miongoni mwetu na kubadilisha asili yetu, na kutufanya tutake kuishi kama Yeye.

⁶³ Mungu, kabla hajafanya jambo lolote, daima hulitangaza Mbinguni kwanza na kisha duniani. Hakuna mtu anayeingia hukumuni bila kuonywa kabisa. Loo, ningetaka kusimama hapa kwa nusu saa ama robo tatu, lakini siwezi na kisha nifanye mstari wa maombi, kuwaacha mwamke kwa wakati unaofaa asubuhi, mwende kanisani.

⁶⁴ Lakini angalieni, hakika, kuna kitu kitakachofuata uamsho huu, Mungu daima hutuma rehema kabla ya hukumu. Daima amefanya hivyo, daima atafanya hivyo. Na uamsho huu mkuu, ambao Kanisa limekuwa nao, uamsho wa miujiza, na uponyaji wa Kiungu, na karama za Roho, kumbukeni, jambo fulani huufuata huo, Mungu daima hutuma rehema kabla ya hukumu. Anaitangaza katika mbingu juu, kama vile wale mamajusi walivyoiona ile nyota, wakaja kumwabudu Bwana Yesu. Halafu basi, Mungu daima hushuhudia yale anayofanya.

⁶⁵ Sasa, tunaona ya kwamba Yesu, wakati huu mkuu, Yeye aliwachagua watu watatu. Sikuzote ninapenda kuwazia juu ya Petro, Yakobo, na Yohana, alipomfufua binti ya Yairo, alimchukua Petro, Yakobo, na Yohana, na hao ni tumaini, imani, na upendo; hao watatu ni mashahidi. Tatu ni ushahidi katika Agano la Kale. Na kwa hiyo wakati huu, tukio hili lilikuwa kubwa sana, na ujumbe ilibidi uwe mkubwa sana, hata Mungu akashuhudia.

⁶⁶ Hilo ndilo tunaloshukuru usiku wa leo, kile ninachomshukuru sana Mungu, kwamba ujumbe huu wa Kipentekoste tunaohubiri, Mungu hutuma ushahidi. Biblia

ilisema katika Waebrania 11, “Mungu huzishuhudia sadaka Zake.”

⁶⁷ Kama mtu akisema lolote, mtu anaweza kusema lolote, bali kama Mungu haliungi mkono kwa Neno Lake na kwa Uwepo Wake, basi yeye hana ushahidi. Kwa hiyo kile asemacho, kama ni, kama akikisema, Biblia inakisema, na Roho anakithibitisha, hao ni mashahidi watatu, basi ni kweli, kimethibitishwa, Mungu anasema kwamba ni kweli.

⁶⁸ Loo, ndipo tunamwona Mungu, tukio hili lilikuwa kubwa sana, Yesu alichukua imani, tumaini, na upendo: Petro, Yakobo, Yohana, kisha wakapanda mlimani. Sasa, huu ulikuwa ni wakati maalum sana mpaka Yeye alikuwa na mashahidi watatu wa kimbunguni pale pia: Eliya, Musa, na Yesu. Watatu duniani, watatu Mbinguni, Yeye alikuwa akienda kuwa kitu ambacho alitaka kirekodiwe na kukumbukwa.

⁶⁹ Sasa, tunapona ya kwamba baada ya wao kuangalia juu na kuona ya kwamba kivuli kilikuwa kimemfunika, kwa kweli kile Mungu alichokuwa akifanya kilikuwa katika Agano la Kale, kama vile ndugu wahudumu wanavyojua, ilikuwa ni kumweka Mwana mahali pake.

⁷⁰ Sasa ninataka, nadhani asilimia tisini ya kusanyiko hili ni la Kipentekoste, kwa hiyo ninataka, ninatumaini tu siudhi, lakini na—napenda tu kufanya wa—wazo hapa, lililo moyoni mwangu. Sasa, mahali tulipofanyia kosa katika milki zetu za Kipentekoste ni wakati tulipofanyika wana wa...binti za Mungu, tumejazwa na Roho Mtakatifu, tukaketi chini, hapo ndipo tulipofanyia kosa baya sana. Mbona, unajiandaa tu kuingia kazini basi. Kama kila mtu aliye na ubatizo wa Roho Mtakatifu angewaka moto, kama Stefano na kama wale wa siku hizo, uamsho ungeenea nchini.

⁷¹ Kwa hiyo, wasema, “Vema, niliokoka, na kutakaswa, na kujazwa na Roho Mtakatifu, na yote yamekwisha sasa.”

⁷² Kama Mungu alifanya hivyo kwa ajili yako, Yeye alikuchagua tu na kukuteua kwa ajili ya huduma Yake uingie kazini. Nendeni mitaani, naam, mshuhudie, shuhudieni habari Zake, hivyo ndivyo hasa tunavyopaswa kufanya.

⁷³ Huko nje kwenye Visiwa vya Karibe, si muda mrefu uliopita, nilisema jinsi Mungu alivyofanya jambo kuu. Kwa namna fulani nilikuwa nikiwatikisa Wafanyabiashara Wakristo, wala sikufanya hivyo hadharani, niliwaweka peke yao, nami nikasema, “Wengi wenu sana mnashuhudia, ‘Mungu alinipa Kadilaki tatu, pia nilikuwa na biashara ndogo, hapa nje pembeni, Naye akanipa Kadilaki tatu na *hii* kubwa mno, na yote *hayo*.’

⁷⁴ “Sana sana ni kuhusu biashara yenu, shuhudieni juu ya Mungu, yale Kristo aliyowafanyia. Toa nafasi, si kile... Tunazidi kuwa wakubwa kupita kiasi, tume—tume—tumepanuka sana

kifedha. Tunachotaka kufanya ni kutoa kitu ambacho tunaweza kumpa Mungu sifa.” Nikasema, “Ni tofauti jinsi gani na Wapentekoste leo, kuliko ilivyokuwa katika siku za Biblia! Waliuza kila kitu walichokuwa nacho na kuwagawia, wakawapa mitume nao wakagawana wao kwa wao.”

Ndipo jamaa fulani mdogo, ndugu mzuri, mtu mzuri sana, akasema, “Ndugu Branham, hapo ndipo walipofanyia kosa kubwa sana walilowahi kufanya.”

Nami nikasema, “Vipi, bwana?”

⁷⁵ Akasema . . . Tulikuwa tumeketi chini ya mbalamwezi kando ya kidimbwi cha kuogelea, tulikuwa huko Kingston, Jamaika, naye akasema, “Hapa ndipo walipofanyia kosa: Ndipo baada ya shida kuanza, hawakuwa na nyumba zozote za kuendea, walifanya kosa kwa kuuza nyumba zao.”

⁷⁶ Nikasema, “Roho Mtakatifu kamwe hafanyi kosa.” Nikasema, “Hawakuwa na makazi yoyote ya kuendea, kwa hiyo walienda kote nchini, wakitangaza yale Mungu aliyokuwa amefanya.” Mnaona? Naam, wakihubiri, wakishuhudia, wakitoa ushuhuda. Hawakuwa na nyumba ya kuendea, walikuwa wasafiri na wageni kweli, Uzao wa Ibrahimu. Mungu kamwe hakosei, kamwe. Tunajaribu ku- . . .

⁷⁷ Nikiwaza, binti mkwe wangu pale, nami nilikuwa nikiimba, hivi majuzi usiku, nikienda nyumbani:

Usitamani utajiri wa bure wa ulimwengu huu,
Ambao huoza upesi sana,
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Hayatapita kamwe.

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Loo, nina furaha sana kuushika mkono huo!

⁷⁸ Sasa, katika Agano la Kale, tunasoma mle ndani, naye Paulo akalielezea katika nyaraka mbalimbali, na kadhalika, kwamba mtoto aliyezaliwa katika fa—familia, mara alipozaliwa, alikuwa ni mwana. Sasa, King James katika tafsiri, ambayo inaonekana kuwa ni tafsiri mbaya ya Yohana Mtakatifu 14, ilisema, “*Nyumbani* mwa Baba Yangu mna majumba mengi.” Vema, kweli inasema, “Katika *Ufalme* wa Baba Yangu kuna ikulu nyingi.”

⁷⁹ Lakini sasa, kama ungeangalia hilo, majumba yangewezaje kuwa katika nyumba? “Katika nyumba ndogo ya Baba Yangu mna majumba mengi.” Unaona, fasiri za Kiingereza hubadilika. Sasa, katika siku za wafasiri wa huyo mfalme, nyumba ilikuwa ni ufalme, naye alikuwa ndiye baba wa nyumba hiyo, raia wake wote walikuwa nyumbani mwake, kwa hiyo hivyo ndivyo King James hapo ilivyokuwa katika utaratibu wa Maandiko.

⁸⁰ Kwa kuwa wakati mtu alimiliki eneo kubwa zuri sana, shamba kubwa, alikuwa na wapangaji wengi mahali pote hapa,

naye alikuwa mtu mwenye shughuli nyingi, ilimbidi kwenda mahali mahali. Ndipo basi wakati mwana alipozaliwa nyumbani mwake, hawakuwa na kitu kama tulicho nacho siku hizi, shule za umma, na kadhalika, kama jengo hili zuri la Eisenhower tulilomo usiku wa leo, hawakuwa nacho siku hizo, iliwabidi kukodisha walimu kuwalea watoto wao.

⁸¹ Sasa, mwana alipozaliwa, alikuwa mwana mara tu alipozaliwa, alikuwa ni mwana aliyezaliwa kwenye nyumba hiyo. Lakini hata hivyo, hakuwa na urithi wowote mpaka alipofikia mahali ambapo alikuwa amejithibitisha kuwa ni mwana. Ndipo basi, alipothibitishwa kuwa mwana, basi akafanya mwana mwenye mamlaka katika familia, na sheria ya kufanywa mwana mwenye mamlaka ilimfanya awe mmiliki sawa na baba yake.

⁸² Sasa, hapo ndipo kanisa la Kipentekoste liliposhindwa, walipofanyika wana, walitulia, kasema, “Hili ndilo. Tuna kanisa letu, tuna dhehebu letu, nasi tutaendelea tu kuongeza wengine wengi.” La, hilo silo. Hilo silo. . . “Tutajenga jengo bora zaidi,” hilo ni jema, “tutawaongeza wengine kanisani,” hilo ni jema, bali Mungu alikufanya mwana kukupa jaribio aone jinsi utakavyotenda nalo.

⁸³ Sasa, baba huyu alijaribu kuangalia kote na kutafuta mwalimu bora sana ambaye angeweza kumpata kwa ajili ya mtoto wake. Sasa, huyo alikuwa ni mwanawe naye hakutaka haini fulani akijaribu kumlea mtoto wake, alitaka mtu ambaye angekuwa mwaminifu. Alitaka mtu, si yule angejaribu kupata sifa kwa kumwambia baba yake, “Loo, mwanao anaendelea vizuri,” wakati sivyo. Alitaka mtu ambaye angekuwa mwaminifu, na kumletea taarifa sahihi, na kuona jinsi mtoto huyu alivyokuwa akilelewa. Kwa hiyo angefanya uchunguzi na kutafuta mwalimu bora sana angaliweza kumpata.

⁸⁴ Na huo ulikuwa ni mfano wa yale Mungu aliyokuwa akifanya. Mungu kamwe hakumwagiza mtu kufanya jambo lolote ambalo Yeye Mwenyewe asingelifanya. Hiyo ndiyo sababu Mungu alifanyika mwili na akafa kwa ajili ya mwenye dhambi, kwa sababu aliweka dhambi juu ya mwenye dhambi.

⁸⁵ Sasa angalieni, basi wakati jambo hili lilipotukia, mwalimu angeenda, amfundishe huyo mtoto, amlee, na kuwaletea wazazi taarifa, jinsi mtoto alivyokuwa anaendelea, ama, jinsi hu—huyo mtoto alivyokuwa anaendelea. Sasa, wakati mtoto huyu alipolelewa, hata hivyo alikuwa ni mwana nyumbani, vipi kama mtoto huyu katika umri fulani akianza kutenda mabaya? Sasa, ilibidi mwalimu huyo awe mtu mwaminifu kuleta taarifa sahihi kwa mzazi.

⁸⁶ Sasa, Mungu alipowatuma wanawe, wana na binti, alimchukua Mwalimu, ama Mlezi kwa hao wana na binti, Naye hakuwa askofu, wala hakuwa kadinali, asingeweza kuwaamini,

kwa hiyo alimchukua aliye bora sana Mbinguni kulea Kanisa Lake, Roho Mtakatifu, Yeye ndiye Mwalimu wa Kanisa. Nasi tumegeuka... Yeye ni mwaminifu, Yeye atamwambia Baba yale hasa tunayofanya, hatashikilia jambo moja, atakuwa mwaminifu mbele za Baba, jinsi watoto Wake wanavyoendelea. Sasa, hiyo ndiyo sababu Yeye alimchagua Huyo, hakukuwa na aliye bora zaidi angaliweza kumpata ila kuwa na Roho Mtakatifu.

⁸⁷ Tumechukua mengine yote ila Roho Mtakatifu, hatutaki Roho Mtakatifu atufundishe, tunataka kumwacha askofu atwambie la kufanya, ama ma—makadinali, ama—ama mtu fulani atuambie la kufanya. Haileti tofauti yoyote yale wanayosema, kama ni kinyume na Neno la Mungu na uongozi wa Roho Mtakatifu, msikilizeni Roho Mtakatifu kwa kuwa huyo ndiye Mwalimu wenu. Amina.

⁸⁸ Kama wakisema, “Siku za miujiza zimepita,” na iwe ni uongo, kwa sababu Mungu alisema ni yeye yule, jana, leo, na hata milele.

⁸⁹ Kama wakisema, “Roho Mtakatifu alikuwa tu kwa ajili ya wanafunzi,” Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, “Ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjje.” Hatupaswi kulivuruga.

⁹⁰ Siku moja, nilikuwa nikihubiri juu ya somo la Isaya 1:18, “Je, hakuna zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu?” Na ni kama tu mtu anayefia kwenye vipandio vya mlangoni mwa daktari, akikataa kunywa dawa yake, si kosa la huyo daktari, si kosa la hiyo dawa, ni huyo mtu kwa sababu hatainywa hiyo dawa.

⁹¹ Hivyo ndivyo ilivyo kwa kanisa siku hizi, tunayo zeri, tuna matabibu, tuna dawa, bali wenye dhambi hufia vitini mwao makanisani mwao na kwenda matesoni, kwa sababu wanakataa kuinywa dawa. Si kosa la daktari, si kosa la dawa, ni kosa la huyo mtu ambaye hatakuja. Hiyo ni kweli. Tulipata zeri huko Gileadi.

⁹² Kwenye Siku ya Pentekoste, wakati ile zeri ilipomiminwa, tulikuwa na daktari pale, jina lake lilikuwa Dk. Simoni Petro, naye akaandika maagizo. Naye akasema... Wakasema, “Tufanye nini tupate chanjo ya swali hili la dhambi?” Kulikuwa na wakati ambapo hapakuwapo na chanjo, lakini tunayo sasa. “Kwa hiyo tunawezaje kufanya, kuondokana na hili?”

“Uliwaambia nini, Dk. Simoni Petro?”

⁹³ Alisema, “Tubuni kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea Kipawa cha Roho Mtakatifu, kwa kuwa ahadi hii, maagizo,” haleluya, “maagizo haya,” (Kile maagizo yanachoandika ni Roho Mtakatifu.) “maagizo haya yanafaa kwa kizazi *hiki*, na kizazi

kile, na kila mtu ambaye Bwana Mungu wetu atamwita.” Ni tiba ya dhambi, tiba maradufu, ya dhambi na ugonjwa.

⁹⁴ Sasa, kama ukichukua maagizo...Daktari anayeandika maagizo, ameichunguza dawa hiyo, naye hana budi kuweka sumu mle ndani kuua vijidudu, naye hana budi kutia kiuasumu mle ndani kupachukua mahali hapo, isije ikakuua. Na kama baadhi ya hawa maskini wauza dawa matapeli, ama *wanaodhaniwa* kuwa ni madaktari wakijaribu kuvuruga maagizo hayo, yatamwua huyo mgonjwa. Hiyo ndiyo shida siku hizi, wanaua, wanakufa kiroho, kwa sababu wanaweka kupeana mikono badala ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, nao wanamwua mgonjwa.

⁹⁵ Acha hayo maagizo, Petro alisema ni kwa kila kizazi baada ya hiki, usiyachezee maagizo hayo, yachukue kama yalivyoandikwa. “Roho Mtakatifu,” akasema, “ni kwa kila kizazi baada ya hiki. Toba, ubatizo wa maji, nawe utampokea Roho Mtakatifu.”

⁹⁶ Hatuna haki ya kusema, “Loo, ubatizo wa maji ni sawa, hakika, njoo huku, tutakubatiza, mkono wa kuume wa ushirika, na hilo latosha.” La, bwana.

⁹⁷ Nami nitawaambia, mwajua, jinsi wanavyopata dawa, wanachukua nungubandia, na kumchanja huyu nungubandia na kuijaribia kwake, kama ikifanya kazi, watakupa wewe. Wakati mwingine itakuua, pia, kwa sababu miili yote ya binadamu si kama ya nungubandia. Lakini wakati Mungu alipotaka kujaribu chanjo hii, Yeye kamwe hakuijaribu kwa nungubandia, aliiweka juu ya Mwanawe, nayo ikastahimili. Amina.

⁹⁸ Walipomtemea mate usoni Mwake, Yeye hakusema neno juu yake, walipomwomba aende maili moja, Yeye alienda mbili, kisha katika mauti ikastahimili, na katika ufufuo ikastahimili. Na kila mmoja wa watu hawa alitaka kujua kwa ajili ya chanjo hii. Nayo hiyo hapo.

⁹⁹ Na matokeo yale yale, ambayo hiyo dawa ilileta kwa watu hao...Sasa, dawa itamfanya mtu mmoja kutenda kwa njia moja, na mwingine nyingine, lakini wakati dawa ya Roho Mtakatifu inapokuja, inawafanya kila mmoja kutenda vile vile.

¹⁰⁰ Nimekuwa huko Thailandi, nyingi za sehemu hizo kuu, Afrika Kusini, na kote, mahali watu walipokuwa, hata hawakujua ni upi ulikuwa mkono wa kulia wala wa kushoto, hebu wampokee Roho Mtakatifu, mnajua wanalofanya? Wanafanya jambo lile lile mnalofanya. Kwa hiyo inafanya kazi vivyo hivyo kwa kila mtu. Kuna kitu Fulani kinachoshuka kutoka Mbinguni na kuijaza mioyo yetu, kama upepo wa nguvu ukienda kasi, nao wanatenda jambo lile lile na kufanya jambo lile lile mnalofanya. Hata hivyo, wasingeweza kuzungumza hata neno moja la Kiingereza wala hawajui mkono wa kulia wala wa kushoto, lakini wakati Roho Mtakatifu anapowagusa,

nao wanachukua maagizo haya, ndipo wanapata jambo lile lile unalopata, wanatenda vivyo hivyo. Mungu anataka kuwaokoa watu.

¹⁰¹ Sasa, hapa juu alikuwa akimweka mwana. Kama mwana huyu hakutenda vema, kulikuwa na kasoro fulani. Ndipo ilimbidi kwenda kwa baba yake, na hebu wazieni aibu ya mwalimu akienda kwa baba yake, na kusema, “Bwana, mimi...”

“Loo, mwanangu anaendeleaje?”

Loo, jinsi ambavyo hapana shaka aliona aibu, “Uh, ha—haendelei vizuri sana. Uh, ha—ha—hatasikiliza kamwe.”

¹⁰² Nashangaa Roho Mtakatifu anasema nini anapokuja mbele za Baba pamoja na tabia za baadhi ya watu Wake hapa duniani. Wakati anapopanda kule juu na kusema, inamlazimu kusema, “Baba, binti Zako wanavaa nguo za wanaume, wanakata nywele zao.”

“Vema, kwani sina madaktari wowote?”

“Hakika.”

“Kuna mtu anayewaambia kulihusu?”

¹⁰³ “Naam. Wanakaa nyumbani Jumatano usiku kuangalia *Tunampenda Susie*, ama chochote kilicho kitu hicho. Hawataenda kanisani, wanaenda kuvua samaki Jumapili asubuhi, badala ya kwenda kwenye shule ya Jumapili.” Loo, jamani, jinsi... Vema, anawezaje kufanya lolote na huyo mwana? Yeye ni haini, hafai chochote.

¹⁰⁴ “Naam, wao kabisa, kanisa linacheza roki, hiyo dansi mpya ya kuzimu waliyo nayo kule chini. Baadhi ya hao jamaa wenye mtindo huu hapa wa kukata nywele batamkia wameketi kule juu, wakipiga makelele wanavyopiga. Na, loo, watu Wako wengi wanaliendea moja kwa moja, na—na wengi wa hao *wanaojiita* madaktari wanaliruhusu.”

“Kwani wanafanya nini na maagizo Yangu ya dawa?”

“Loo, wanayapuuza, wanasema yalikuwa ni kwa ajili ya siku nyingine.”

¹⁰⁵ Unafikiri inamlazimu kuwazia nini? Mbona, Yeye hana budi kuwazia ya kwamba wengi wa wachungaji wanavuta sigara, wanakunywa pombe, wanacheza karata. Wazieni hilo. Wanafanya hivyo. Nilisafiri kote nchini na kote ulimwenguni, najua ni kweli. Bila shaka. Loo, ni jambo baya sana. Jinsi ambavyo Roho Mtakatifu hana budi kuona haya mbele za Mungu, kusema jinsi kanisa linavyoendelea! Loo, hapana shaka ni jambo baya sana!

¹⁰⁶ Sasa, mtoto huyo katika Agano la Kale, kamwe hakuwa na urithi wowote. Mbona, baba asingeweza kumwaminia chochote. Angekuwa jamaa wa aina gani? Lakini asingeweza kumtumaini,

daima alikuwa mwana, bali kamwe hakuwa na urithi wowote. Na msipoangalia, kanisa la Kipentekoste, hilo litakuwa ndilo fungu letu, hakuna urithi.

¹⁰⁷ Lakini angalieni, Biblia ilisema ya kwamba ulimwengu, leo hii, unaugua, ukingojea kudhihirishwa kwa wana wa Mungu, wana wa Mungu kudhihirishwa. Ulimwengu unangojea hilo, wakati ujao, ambapo wana wa Mungu, ambao ndio watawala wa dunia...

¹⁰⁸ Mungu aliwaweka watu duniani, mwanadamu apate kuitawala dunia. Biblia ilisema ya kwamba mwanadamu ni mungu mdogo. Mlijua hilo? Hakika ndivyo alivyo. Yesu alisema, “Haikuandikwa katika torati zenu, ya kwamba ninyi ni miungu? Na kama wao ni miungu, manabii, ambao Neno la Mungu liliwajia, mnawezaje kunihukumu Mimi ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?”

¹⁰⁹ Mnaona, wao ni—wao ni—wao ni miungu, miungu walioanguka. Wanapata milki, ulimwengu, wanapaswa kuishughulikia, miti na uhai wa wanyama, kila kitu kinangojea kudhihirishwa kwa wana wa Mungu watakapodhihirishwa duniani.

¹¹⁰ Loo, njoo Bwana Yesu, ndilo ombi langu. Loo, ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu wakati watakapodhihirishwa! Tunajiandaa sasa kwa ajili ya kuja kwa wakati huu, Kanisa halina budi kujiweka tayari.

¹¹¹ Angalieni, tunapoendelea mbele kidogo, sasa, kama huyu mwana alikuwa kwa namna fulani ni mvulana haini, wala hakumtii baba yake, mbona, hu—hu—huyo mwalimu aliona haya, na, mbona, baba asingeweza kumpa chochote. Lakini vipi kama alikuwa mvulana mzuri? Basi wakati baba anaposema, “Mwanangu anaendeleaje?”

¹¹² “Loo,” mwalimu anasema, “Baba, unajua nini? Mvulana wako ni kama wewe kabisa. Yeye anafanya kazi yako, anaifanya jinsi tu wewe ungeifanya. Mbona, ufalme wote hapa, unaweza kuona uakisi wako moja kwa moja katika mvulana huyo!” Loo, jamani! Hilo ndilo tunalotaka. Jambo ndilo hilo, uakisi wa Yesu Kristo.

¹¹³ Katika ulimwengu wa kale, walikuwa wakichukua dhahabu na mpigaji angeipiga, akitwanga takataka kutoka kwake, na jinsi alivyojua alikuwa amezitoa zote, ni wakati uakisi wake mwenyewe unapoakisiwa kwenye hiyo dhahabu, alikuwa ametoa uchafu wote kutoka kwake na takataka zote. Na hivyo ndivyo Mungu anavyolitendea Kanisa Lake, Yeye analipiga kwa nguvu za Injili, akiwaambia, akiwapindua, akiwapa upande *huu*, na upande *ule*, na kuupiga ulimwengu wote utoke, na mashaka yote, mpaka uakisi wa Yesu Kristo utakaporudi Kanisani, ambapo Kanisa linaweza kumwona Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele, mpaka tunaweza kuona huo uakisi, Kanisa

likitenda kazi katika nguvu za Mungu, kama tu vile Yesu alivyokuwa hapa duniani. Anajiakisi Mwenyewe Kanisani.

¹¹⁴ Sasa, jinsi Roho Mtakatifu anavyopanda juu, kasema, “Loo, Kanisa hilo...” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “. . . kwa nini ishara na maajabu na uakisi wa Maisha Yako ni mkamilifu. Wanafanya kila kitu ulichofanya, kama tu ulivyosema. Na hivi wanalizingatia vilivyo? Jamani, wao ni—wao ni watu walio na tabia halisi.” Hivyo ndivyo Biblia inavyotutaka tufanye, hivyo ndivyo Mungu anavyotutaka tufanye, hivyo ndivyo Roho Mtakatifu anavyotutaka tufanye.

¹¹⁵ Kama nilivyokuwa nikisimulia kwenye kiamshakinywa hivi majuzi asubuhi pamoja na ndugu, huko chini kusini, ambako walikuwa na utumwa, walikuwa na wanunzi wa kale waliokuja na kununua watumwa kama tu vile unavyonunua magari kwenye—kwenye uwanja, wanapata leseni ya mauzo kwa ajili yake. Anauza maisha ya binadamu namna hiyo, kama watumwa.

¹¹⁶ Mungu alimfanya mwanadamu, mwanadamu akawafanya watumwa. Mungu hakukusudia mtu yeyote awe mtumwa wa mwingine, sijali jamii yake, rangi, wala kanuni ya imani. Wewe si mtumwa, wewe ni mtumishi wa Mungu aliyezaliwa huru. Hataki mtu yeyote awe mtumwa, hakuna kitu cha kututawala ila Yeye Mwenyewe.

¹¹⁷ Kwa hiyo wangepita na kuchukua baadhi, labda mtu ambaye alikuwa mkubwa, mwenye nguvu, aliyekuwa na maskini mke mdogo, mwembamba, wakamtenganisha naye, wakamzalisha na mwanamke mkubwa, mzito, wapate watumwa bora zaidi. Mbona, ilikuwa ni uovu, kama wanyama! Hao watu ni watu. Kwa sababu rangi yao ilikuwa tofauti. . . Yesu Kristo alikufa apate kuwaokoa watu hao, ni wanadamu kama mtu mwingine yeyote.

¹¹⁸ Nao wangepitia pale, basi siku moja dalali alipitia hapo na kusema, kwenye shamba la kale, “Ningependa ku—kuona una watumwa wangapi.”

Kasema, “Nina kama mia moja.”

¹¹⁹ Naye akaenda huko nje, nao watumwa wako mbali na nyumbani, walikuwa na huzuni, walijua kamwe hawangewaona baba na mama tena, hawangewaona watoto wao tena. Wa—wangechukua mijeledi na kuwacharaza wapate kufanya kazi. Nao wakamwona kijana mmoja pale, haikuwabidi kumcharaza, kifua mbele, kidevu juu, alitembea kwa majivuno. Na kwa hiyo huyo dalali akasema, “Ningetaka kumnunua mtumwa huyo.”

“Loo,” akasema, “hauzwi.”

Akasema, “Aisee,” akasema, “hivi—hivi yeye ni bosi juu ya hao wengine?”

Akasema, “La, yeye ni mtumwa.”

Akasema, “Labda unamlisha tofauti na unavyowalisha hao wengine.”

Kasema, “La, wote wanakula kwenye manchani pamoja huko nje.”

¹²⁰ Kasema, “Ni kitu gani kinachomfanya tofauti sana na hao wengine? Jamani, yeye ni chapchap sana! Haikubidi kumcharaza, yeye amezamia kazini moja kwa moja wakati wote.” Kasema, “Kwa nini iko hivyo?”

¹²¹ Akasema, “Nilishangaa, pia, mpaka nilipogundua.” Kasema, “Katika nchi ya uenyeji wake baba yake ndiye mfalme wa hilo kabila, na ingawa yeye ni mgeni mbali na nyumbani, lakini bado anajua yeye ni mwana wa mfalme, naye anatenda kama mwana wa mfalme.” Haleluya!

¹²² Hivyo ndivyo kanisa la Kipentekoste linavyopaswa kufanya, hata hivyo, tunadhihakiwa na kubandikwa jina la kila namna linaloweza kuwa, inatupasa kuenenda kama wana na binti za Mungu, kwa sababu Mungu ndiye Mfalme wetu. Wanawake wanapaswa kuvaa na kutenda kama kina mama wa heshima, wanaume wanapaswa kuwa wanaume, wanapaswa kuwa wana na binti za Mungu, tabia yetu, ushuhuda wetu unapaswa kusimama juu sana mjini.

¹²³ Biblia ilisema ya kwamba “Ninyi ni chumvi ya dunia.” Chumvi ndiyo ladha kama ikigusa. Hebu weka chumvi *hapa*, na nyama *pale*, kamwe hutaiokea hiyo nyama, inakubidi kuweka chumvi na nyama pamoja. Nayo chumvi husababisha kiu, nawaambia tunachohitaji usiku wa leo ni kukolea chumvi sana, mpaka tuwafanye wanaume na wanawake waone kiu ya kuwa kama ninyi. Endelea, useme, “Pale, kama kuliwahi kuwa na Mkristo, siendi kanisani mwake, lakini huyo mwanamke kweli ni Mkristo. Yule *pale* mwanaume, siendi kanisani mwake, ninaenda kanisa lingine, lakini kama kuliwahi kuwa na Mkristo, yule pale mmoja wao.”

¹²⁴ Hilo ndilo tunalotaka. Huyu ndiye aina ya mtu ambaye Mungu anamtaka Roho Mtakatifu amletee taarifa. Loo, kama huyo mvulana alikuwa ni mvulana mzuri, ninii yake, maisha ya Mungu yakiakisiwa ndani yake, maisha ya baba yake yanaakisiwa ndani yake. Sasa, sisi ni wana wa Mungu, basi Mungu anapaswa kuakisi Maisha Yake ndani yako. Yesu alisema, “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi, lakini kama nikizitenda kazi za Baba Yangu, ziaminini hizo kazi.”

¹²⁵ Haya basi, tunapaswa kuwa tukiyaakisi Maisha ya Mungu maishani mwetu. Mungu anapaswa kuakisi, tunapaswa kupiga na kuondoa, mashaka yetu yote na kila kitu kutoka kwetu, kufikia ambapo, mpaka wakati Mungu anapotaka kusema, “Sasa, angalieni mmoja wa watoto Wangu *pale*, ana *hiki-na-hiki*. Mmoja Wangu *hapa*, hatashikwa na mfurukuto na kuendelea kurukaruka mahali mahali, anaamini Neno Langu. Anasimama pale pale, moja kwa moja huko juu. Naam, bwana. Hakuna

kitu kinachoweza kumfanya abadilike, kwa sababu anayaakisi Maisha Yangu.”

¹²⁶ Sasa, sikilizeni sasa, ndugu wanaoketi hapa, kama mvulana huyo alikuwa ni mvulana mzuri kulikuja siku, loo, jamani, siku fulani mpaka kukafanywa sherehe iliyofanyiwa mvulana huyo. Basi mvulana huyo alipelekwa nje kwenye uwanja wa umma na kuvikwa vazi fulani la kifalme, nao wakafanya, baba alifanya, wakafanya sherehe ya kufanywa mwana mwenye mamlaka, naye akampa mamlaka mwanawe aliyekuwa amezaliwa.

¹²⁷ Sasa, unapompokea Roho Mtakatifu, hilo ni jambo moja, unazaliwa, lakini sasa kwa ajili ya sherehe ya kufanywa mwana mwenye mamlaka. Ndipo akampa mamlaka mvulana huyu katika familia yake, nao wakafanya sherehe. Sasa, kama wangeandika hundi, chochote alichofanya mvulana huyo, kilikuwa halali tu, jina lake lilikuwa halali tu kwenye hundi kama la baba yake baada ya kule kufanywa mwana mwenye mamlaka. Alikuwa mrithi baada ya kufanywa mwana mwenye mamlaka.

¹²⁸ Vema, hapo ndipo Kanisa linapopaswa kuwa usiku wa leo, linapaswa kufikia mahali ambapo Mungu atakuita uende mahali fulani, na kukufunika kwa utukufu Wake, aeneze nguvu Zake juu yako, akufanye mwana mwenye mamlaka, na kukuweka mahali pako, utukufu, katika ule Mwili ambapo unaponena, jambo fulani linatukia. Hicho ndicho Kanisa linachohitaji usiku wa leo. Lakini kama sisi, tabia zetu zikishuka badala ya kwenda juu, Yeye atafanyaje jambo hilo?

¹²⁹ Hatuna budi kuendelea kuamini kila kazi ya Mungu, na kuitafuta haki, na kufanya yaliyo mema machoni pa Mungu, tukimwita Yeye kila siku, kila siku kuhusu kazi Yake, tukiwafanya wengine kuja kanisani, tukijaribu kumfanya mtu fulani aje amtumikie Bwana. Watu wote unaowafanyia kazi, muuza maziwa, m—mtu wa posta, na—na—na mtu wa aiskrimu, ama yeyote yule, wote unaokutana nao, ongea nao juu ya Bwana. Iongee kwa maneno yaliyokolea, kwa utamu, ambapo, usiwarukie, inene tu kwa utamu, hata watasema, “Aisee, mama huyo ni mama halisi. Alininenea habari za Bwana. Mwanamume huyo, sijawahi kumwona mwanamume kama huyo. Yeye ndiye mwanamume mzuri kuliko wote niliyepata kukutana naye. Mnajua, ningetaka kuwa na dini yake.”

¹³⁰ Hivyo ndivyo wanavyowazia kuhusu dini yake, bali dini ni kifuniko. Hiyo ni kweli. Na kifuniko chetu si, “Sisi ni Wamethodisti, Wabatisti, Wapresbiteri, Wapentekoste.” Kifuniko chetu ni Damu ya Yesu Kristo, hiyo ndiyo kifuniko chetu, dini yetu.

¹³¹ Sasa, angalieni hili, basi wakati huku kufanywa mwana mwenye mamlaka kulipokuja, jina la mvulana huyo lilikuwa ni

kama tu la baba yake. Alikuwa mrithi wa vitu vyote wakati huo, vyote aliyokuwa navyo baba yake, yeye alikuwa navyo pia.

¹³² Sasa, Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo, yeye naye atazifanya. Yeye ataweza kufanya mambo yale yale ninayofanya.” Sasa, Mungu alikuwa akithibitisha hapa, yale aliyokuwa akimfanyia Mwanawe Mwenyewe, alikuwa amempendeza.

¹³³ Sasa angalieni, wote walikuwa wamesimama pale, na lilikuwa ni jambo kuu, ndipo Mungu akawaita mashahidi watatu wa Mbinguni, na mashahidi watatu wa duniani, kulishuhudia, kwamba, kama ilivyo katika Agano la Kale, walikuwa na mashahidi huko nje kuhakikisha kwamba huku kufanywa mwana mwenye mamlaka kulikuwa kumefanywa. Sasa, Mungu alimfanyia nini Mwanawe? Walitoka wakaenda kule kwenye mlima huu na kwa ghafla, likaja wingu kubwa jeupe na kumtia Yesu uvuli, ndipo mavazi Yake yakametameta kama jua, mavazi Yake. Ilikuwa ni kitu gani? Lile vazi maalum la kufanywa mwana mwenye mamlaka, amina, vazi maalum la kufanywa mwana mwenye mamlaka. Naye akamtia uvuli, na kusema, “Ninampa Mwanangu mamlaka. Huyu ni Mwanangu mpendwa, msikieni Yeye, Yeye Ndiye.”

¹³⁴ Loo, mnajua wakati mambo ya kimbinguni yanapofanywa, hu—huwafanya watu wasisimkwe. Hilo ndilo lililotukia katika uamsho wetu, katika uamsho wa Kipentekoste, sisi... daima hufanyika hivyo.

¹³⁵ Musa alipopanda kutoka Misri, mambo ya kimbinguni yalikuwa yamefanywa, wasiotahiriwa waliambatana naye, wakaichafua hiyo kambi baada ya kitambo kidogo. Nasi tumekuwa na watu wengi sana wa kujaribu kuiga kuwa na Roho Mtakatifu. Watu ndio kwanza waseme, “Vema, hao wengine walipaza sauti, nitapaza sauti, pia.” Huo ni mwili.

¹³⁶ Nawe unaweza kufanya lolote la uigaji huo, lakini huyo bado si Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ni jambo linalotukia *hapa* ndani, jambo ndilo hilo, linalozaa matunda. Kama nilivyosema jana usiku, “Kondoo huzaa sufu, kwa sababu yeye ni kondoo. Nawe ukizaliwa mara ya pili, unazaa tunda la Roho kwa sababu Mungu yuko ndani yako.” Unaona?

¹³⁷ Sasa, jambo fulani lilitukia. Musa alikuwa na umati uliochanganyika, daima ni umati uliochanganyika, tumekuwa na umati uliochanganyika, umetoka kwenda kuiga karama, na—na kuninii, umewafanya watu kuogopa.

¹³⁸ Sasa, nikizungumza kwenye kiamshakinywa hivi majuzi asubuhi na hao ndugu, siwezi kuwalaumu wachungaji kwa kuogopa, kila kitu ulimwenguni kimeachiliwa. Hiyo ni kweli kabisa. Loo, mihemko ya kila namna ambayo si ya kimaandiko, na chochote kile, na upuuzi mwingi ambao hata si wa Kimaandiko. Siwalaumu wachungaji, wao ni wachunga kondoo,

Mungu atawawajibisha kwa jambo hilo. Lakini dola bandia inamaanisha nini? Dola bandia inamaanisha ya kwamba hiyo imefanyizwa kutokana na iliyo halisi, kuna iliyo halisi mahali fulani. Kwa nini ukubali ya bandia, wakati kuna, anga zote zimejaa za Kipentekoste zilizo halisi? Hilo ndilo linalonishangaza. Kwa nini unataka kukubali kibadala, wakati anga zimejaa nguvu *halisi* za Kipentekoste, bila shaka, ambazo huusafisha moyo kabisa?

¹³⁹ Sasa, mnajua Petro alisisimkwa wakati mambo ya kimbinguni yalipofanywa, alimwona Yesu ametukuzwa pale, naye Mungu akimfanya mwana mwenye mamlaka. Sasa, wakati baba alipompa mwana mamlaka, katika Agano la Kale, huyo mwana alikuwa kiongozi, hiyo ni kweli, alipelekwa kule. Sasa, Mungu alisema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa ambaye ninapendezwa Naye, tangu sasa na kuendelea, msikieni Yeye. Msikieni Yeye.”

¹⁴⁰ Petro alisisimkwa, akafanya kama wanadamu wafanyavyo, wakati mambo ya kimbinguni yanapofanyika, akasema, “Hebu na tujenge vibanda vitatu hapa, hebu na tuunde madhehebu matatu kutoka kwake. Ndipo wale wote wanaotaka kuabudu chini ya torati, na wote wanaotaka kuabudu chini ya manabii, na wote wanaotaka kumwabudu Yesu, tutakuwa na madhehebu matatu mbalimbali.”

¹⁴¹ Hivyo ndivyo inavyoenda, una mvua za masika, mvua za vuli, mvua za ndani, mvua za nje, na mambo ya kila namna yanaifuata, hiyo ni kweli, hiyo ni kweli. “Hebu na tuunde baadhi ya madhehebu.”

Lakini kabla hajamaliza kunena, kabla hajalitoea kinywani mwake, Mungu alisema, “Huyu ni Mwanangu.”

¹⁴² Kulikuwako na Musa, yeye aliwakilisha torati. Vema, sheria—sheria ni polisi, sheria itakutia gerezeni, haina mamlaka ya kukuachilia, sheria inakuhukumu tu, sheria ilituleta hukumuni, sheria inakuhukumu. Nina furaha kwamba Musa na torati zake ametoweka, haikuwa na neema ndani yake, haikuwa na ukombozi ndani yake, ilikuwa ni sheria ya adhabu kwamba wewe una hatia, torati ilisema. Kukuweka gerezeni, hivyo tu, uko gerezeni. Nina furaha kwamba hiyo imepita.

¹⁴³ Halafu basi, hapo alisimama Musa, ama, yule—yule Eliya, Eliya aliwakilisha manabii ambao walikuwa ni haki ya Mungu. Eliya alipanda mlimani, akaketi chini. Ndipo mfalme akatuma kundi la watu kumkamata. Akasimama na kusema, “Mungu aliniambia nije hapa na kuketi chini, msije kwenye maeneo haya.” Kasema, “Kama mimi ni mtumishi wa Mungu, Moto na ushuke kutoka Mbinguni na kuwateketeza.” Moto ukashuka. Hiyo ni haki. Wasingelisikia Neno, kwa hiyo hiyo ni haki. Ndugu, nina furaha, sitaki haki Yake, nataka rehema Yake si haki Yake.

¹⁴⁴ Sote tumehukumiwa na sheria Yake, sote tungekufa chini ya haki Yake. Nina furaha sana kwamba Mungu alisema, “Wameondoka tayari, Huyu ni Mwanangu mpendwa, msikieni Yeye.” Yeye ana rehema, upendo, neema, uponyaji, utukufu, na nguvu, na Roho Mtakatifu kwa ajili yetu. “Msikieni Yeye, Huyu ni Mwanangu mpendwa. Alijeruhiwa kwa makosa yako, akachubuliwa kwa maovu yako, adhabu ya amani yako ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake wewe uliponywa. Msikieni Yeye. Njoni Kwangu ninyi nyote msumbukao, na wenye kulemewa na mizigo, nitawapa pumziko.”

¹⁴⁵ “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo, yeye naye atazifanya. Kubwa kuliko hizi atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba Yangu. Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo, nanyi mtapewa.” Loo, jamani! “Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata mwisho wa ulimwengu, hata ukamilifu wa dahari.” Haleluya!

“Huyu ni Mwanangu mpendwa, msikieni Yeye.”

¹⁴⁶ Mkitaka uponyaji: Msikieni Yeye. Mkitaka rehema: Msikieni Yeye. Mkitaka Roho Mtakatifu: Msikieni Yeye. Usipeane mikono na askofu, gusa vazi *Lake*. Ukitaka uponyaji, msikie Yeye. Kama daktari akisema utakufa, msikie Yeye. Msikie Yeye. Msikieni Yeye! Inatosha kumsisimua mtu.

¹⁴⁷ Petro alikuwa ameona kitu halisi, jambo fulani lilitukia ambalo lilikuwa ni la kweli. Na mwanamume yeyote aliye na tabia, mwanamke yeyote aliye na tabia, wanataka, ulimwengu una njaa ya kusikia kitu halisi. Wanataka kupata kitu ambacho ni halisi, wakikipata, wako tayari kukipokea. Lakini wanataka kitu ambacho ni halisi, si udanganyifu fulani, kujifanya.

¹⁴⁸ Ninyi nyote mnajua ya kwamba mimi ni mwindaji. Nilikuwa nikienda kuwindia kwenye misitu ya kaskazini miaka mingi iliyopita. Nilikuwa na kibanda kule juu ambacho kilikuwa ni cha jamaa mwingine, mimi na yeye, nasi tuliwinda. Jina lake lilikuwa Bert Call, mmoja wa wawindaji bora sana niliopata kuona, na mtu katili kuliko wote niliyepata kumjua. Huyu mtu alikuwa ndiye mtu katili kuliko wote, niliyepata kumwona maishani mwangu. Naye alikuwa... Tulikuwa tukiwinda pamoja naye, lakini alikuwa—alikuwa hodari wa shabaha, nusu Mhindi, pia, na usingeweza kumpoteza mwituni, haikukulazimu kwenda kumtafuta mahali fulani, yeye alikuwa—daima alikuwa chonjo. Lakini alikuwa tu na moyo katili sana, naye alikuwa na macho yaliyoonekana kama ya mjusi. Naye angeninii, sikuzote alipenda tu kunitania kuhusu kuwa mhubiri. Na, mwajua, alikuwa akiwapiga risasi maskini watoto wa kulungu apate kuniudhi.

¹⁴⁹ Sasa, ninyi mnaowinda, ninyi ndugu mnaowinda, sina neno dhidi ya kumpiga risasi mtoto wa kulungu. Kama sheria inasema unaweza kumchukua, sawa, lakini usipige risasi kundi kubwa lao kikatili. Hakuna kitu katika kumwua mtoto wa kulungu, hilo ni sawa. Ibrahimu alimwua ndama, naye Mungu akamla. Ili kwamba, si... Makosa hayapo hapo, bali ni kuwa tu katili, ni mtazamo wako. Hiyo ni kweli. Naye alifanya hivi tu kikatili, alitaka kunifanya nijisikie vibaya.

¹⁵⁰ Mwaka mmoja, mimi na mke wangu tulipanda kambini, nami nilichelewa kidogo kwenda huko, maana ilinibidi kufanya kazi nimechelewa, naye alikuwa amejitengenezea maskini filimbi ndogo iliyolia kama tu mtoto mdogo wa kulungu anayemlilia mama yake, naye angepiga filimbi hiyo. Nikasema, "Bert, hutatumia hiyo."

Akasema, "Loo, ewe mhubiri mwoga kama kuku, rudia fahamu zako."

¹⁵¹ Nikasema, "Bert, hakika usingefanya hivyo, rafiki." Nikasema, "Wewe ni mmoja wa jamaa bora sana niliopata kukutana nao, mwindaji mzuri, ninapenda kuwa pamoja nawe, lakini wewe ni katili sana." Nikasema, "Usiwapige risasi hao watoto wachanga namna hiyo." Nilimwona akipiga risasi mmoja siku moja, alikuwa akila matofaa, akayalipua hayo matofaa, akamrusha huyo mtoto wa kulungu kwa mamaye upande wa pili na kumwua. Nikasema, "Loo, ungewezaje kufanya hivyo? Wewe ni jamaa mwenye moyo katili."

¹⁵² "Loo," akasema, "wewe una moyo wa kuku tu, mhubiri, hivyo ndivyo mlivyo ninyi wahubiri wote, waoga tu kama kuku." Nikasema... Akasema, "Nilidhani ulikuwa ni mwindaji."

¹⁵³ Nikasema, "Mimi ni mwindaji, ila si mwuaji." Nikasema, "Huyo ni mwuaji, huyo ni mbaya kama Hitler," nikasema, "kufanya jambo kama hilo."

¹⁵⁴ Loo, tukaenda kuwinda siku hiyo, na ilikuwa mwishoni mwa msimu, na—na hao kulungu wenye mkia mweupe kule juu, mnafikiri Houdini alikuwa ni bingwa wa kutoroka, unapaswa kumwona mmoja wao baada ya bunduki chache kufyatuliwa, na kwa kweli ni vigumu kuwapata. Kulikuwa na kama, loo, nadhani, kama futi moja na nusu ya theluji ardhini, hali nzuri ya hewa ya kufuatilia.

¹⁵⁵ Nasi tulitoka mbali kabisa, tukaenda mpaka adhuhuri, na daima tuliweka chupa ya themosi iliyojaa chokoleti moto, ina changamko kubwa kwake, na sambusa kadhaa, na yapata adhuhuri tungeketi na kula sambusa hizi tulipopanda juu ya Mlima Cherry, na—na juu ya Safu ya Rais, na kadhalika. Ndipo tungerudi chini kupitia yale mapengo, yeye angechukua njia moja, nami nyingine tukirudi kambini, tuingie usiku huo.

¹⁵⁶ Kwa hiyo, tulikuwa tumewinda asubuhi nzima, kidogo muda ulikuwa umeenda sana mchana, nasi tulikuwa tumepitia

kwenye upenyo mdogo, yapata tu ukubwa wa jumba hili la mikutano. Sasa, mtu yeyote anayewinda kulungu anajua yapata saa tano mchana, kulungu wamelala chini. Na hasa sana kama wamewindwa sana, wanajificha, wanakaa mle na kujiua kwa njaa, ama kula kwa mwangaza wa mbalamwezi. Halafu basi, wao... Ni vigumu kuwapata. Na kama wakitoka kamwe, itakuwa jioni sana, mapema sana asubuhi. Wanarudi kwenye hicho kichaka na mabonde na kujificha. Maskini hao mikia myeupe ni hodari sana kwa hilo.

¹⁵⁷ Kwa hiyo tukasimama hapo, hata hatukuwa tumeona mburuzo. Ndipo Bert kwa namna fulani akainama chini, nilikuwa kwenye chungu cha theluji, naye akainama chini, akaingiza mkono kwenye shati lake, nikawaza, “Vema, yeye anaiendea chupa yake ya themosi sasa, tutakula sambusa.” Basi nikaweka bunduki yangu chini. Ndipo alipotoka, aliniangalia kwa hayo macho ya mjusi, na alikuwa na maskini filimbi hii ndogo.

Nikasema, “Bert, hutaipiga hiyo!”

Akasema, “Loo, mhubiri rudia fahamu zako.”

¹⁵⁸ Ndipo akapuliza filimbi hiyo ndogo, nayo ikasikika kama mtoto mdogo wa kulungu anayemlilia—anayemlilia mama yake. Basi alipofanya hivyo, upande wa pili tu wa huo upenyo mama mkubwa wa kulungu akasimama, sasa, kulungu jike ni mama kulungu, akasimama. Alikuwa karibu sana, hata ningeweza kuona hayo macho makubwa, ya hudhurungi, na hayo masikio makubwa mno, namna *hiyo*, yamesimama. Alimsikia mtoto huyo mchanga, alikuwa ni mama, naye mtoto alikuwa hatarini, akalia.

¹⁵⁹ Akakanyaga kidogo kwa kishindo, maskini Bert akaniangalia tena, nikasema, “Loo, usifanye hivyo, Bert.” Ndipo akaipiga tena, naye akajitokeza moja kwa moja kwenye uwazi.

¹⁶⁰ Sasa, ndugu, hilo si kawaida kwa kulungu huyo. Nami karibu ningeweza kuona mishipa usoni mwake, kitu hicho kikubwa, kizuri kimesimama pale. Nami nikamwona maskini Bert akitia risasi hiyo, hiyo .30-06 kule juu, akainua bunduki hiyo, yeye ni hodari sana wa shabaha, huo unywele wa darubini ulilenga moja kwa moja kwenye moyo wake mwaminifu.

¹⁶¹ Sasa, yeye hakuwa akiigiza tu, kulikuwa na kitu fulani ndani yake, kulikuwa na mama, huyo mtoto alikuwa hatarini. Wakati bolti ilipoanguka, huyo kulungu alisikia hiyo bolti ikianguka, wakati alipovuta bolti juu yake, risasi, ikaalika kwenye mtutu kutoka kwenye chemba, basi wakati ilipoalika chini namna *hiyo*, aligeuka na kuangalia, naye akamwona huyo mwindaji.

¹⁶² Ilinibidi tu kuinamisha kichwa changu. Akaangalia. Kwani mnafikiri alikimbia? La, bwana. Alimwona huyo mwindaji, akamtazama kwa dakika moja, kisha akageuka, akijaribu kutafuta mahali mtoto huyo mchanga alipokuwa. Yeye hakuwa

mnafiki, alikuwa ni mama, kulikuwa na kitu ndani yake, bila kujali kuishi au kufa, mtoto wake alikuwa hatarini, na afe asife, atamtafuta mtoto huyo.

Nami nikasema, “Bert, hutafanya hivyo!”

¹⁶³ Nikamwona akilenga, nilijua katika sekunde moja ama mbili angeulipua huo moyo mwaminifu wa mama huyo moja kwa moja hata upande wake mwingine, risasi hiyo kubwa, ya mia moja na themanini, ya uyoga, ingeulipulia moyo wake hata upande huo mwingine.

¹⁶⁴ Nikawazia, “Bert, unawezaje kuwa katili hivi, kufanya jambo kama hilo, kuulipua moyo huo mwaminifu wa mama huyo, akisimama pale kwa moyo halisi na mwaminifu?” Hata alipokabiliwa na mauti, hakujali. Mtoto wake alikuwa hatarini, mwindaji arushe risasi asirushe angemtafuta mtoto huyo. “Ungewezaje kuwa katili hivi kufanya hivyo?”

¹⁶⁵ Hakuwa akiniona, alikuwa analenga chini, nami nilijua alikuwa hodari wa shabaha. Niligeuza tu mgongo wangu, nisingeweza kuangalia likitendeka. Nikaanza kuomba kimoyomoyo, nikawaza, “Bwana, usimwache afanye hivyo, usimwache amwue huyo mama wa thamani hapo, angalia anachofanya, akitembea pale nje akimtafuta mtoto wake mchanga. Ni tendo la kinafiki kumfanya afikiri ya kwamba mtoto wake mchanga yuko huko nje, na kumleta pale nje, huo moyo mwaminifu, akimwinda mtoto wake mchanga, kisha uulipue moyo wake, huo ni ukatili.” Nikasema, “Usimwache afanye hivyo, Bwana.”

¹⁶⁶ Nilingojea wala hiyo bunduki haikufyatuka, nikashangaa imekuwaje, basi nilipogeuka, bunduki ilikuwa ikienda *hivi*, akitetemeka.

¹⁶⁷ Akaangalia kote, macho hayo ya mjusi yalikuwa yamebadilika, machozi makubwa yalikuwa yakitiririka mashavuni mwake, akaitupa bunduki hiyo chini ardhini, akanishika kwenye mguu wa suruali, akasema, “Mhubiri, nimetosheka nayo.” Kasema, “Niambie kuhusu huyo Yesu unayemjua vizuri sana.”

¹⁶⁸ Ilikuwa ni kitu gani? Aliona kitu halisi. Mahubiri yote niliyokuwa nimemhubiria, nyimbo zote alizokuwa amesikia... Yeye ni shemasi katika kanisa la Kibaptisti huko juu sasa. Shida ilikuwa ni nini? Alipoona kitu halisi, aliona kitu ambacho hakikuwa cha kinafiki, aliona kitu kilichokuwa kimewekwa hadharani. Yesu alisema, “Wakinyamaza, miamba itapiga kelele mara moja.”

¹⁶⁹ Ndugu, dada, watu wanataka kuona kitu ambacho ni halisi. Wanataka—wanataka kitu ambacho wanaweza kuona ambacho ni cha kweli. Naye Mungu anacho kwa ajili yako usiku wa leo, huyo ni Mwanawe mpendwa: Msikieni Yeye. Yeye Ndiye anayeweza kukupa hicho kilicho *halisi*, si kitu fulani,

unachosema, “Vema, Mkristo anapaswa kutenda *hivi*,” bali onyesho halisi la Ukristo halisi.

¹⁷⁰ “Huyu ni Mwanangu mpendwa, msikieni Yeye,” alisema Bwana.

¹⁷¹ Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi. Huku mmeinamisha vichwa vyenu, kwa muda kidogo tu, nitakuuliza swali aminifu, nami ninataka unyofu wa moyo wako. Sasa, acheni tu mimi na Roho Mtakatifu pekee tuangalie, tafadhalini, kila mtu akiomba.

¹⁷² Ni wangapi wenu humu ndani wangetaka kumwambia Mungu, “Nifanye Mkristo kiasi hicho kwa ajili Yako, nipe upendo uo huo Kwako ambao maskini huyo mama kulungu alikuwa nao kwa mtoto wake, hata iweje.”

¹⁷³ Mungu akubariki. Mungu akubariki. Loo, angalieni tu kote jengoni, huko juu kwenye roshani, karibu asilimia mia moja, mikono imeinuliwa. Kusema kweli, yangu iko juu, pia.

¹⁷⁴ Mungu, weka ndani yangu kufanya mapenzi Yako. Umba ndani yangu, Bwana, umba ndani yangu njaa kubwa zaidi, umba ndani yangu na Kanisa hili, Mwili Wako, umba ndani yetu Roho ya wana na binti Zako. Tufanye halisi, Bwana, tufanye halisi. Tunakupenda, Baba. Tupe Roho Yako. Tunamsikia akinena nasi usiku baada ya usiku, tunamsikia kupitia Biblia wakati mchungaji akitufundisha, tunamsikia katika karama Zake, anapozungumza akijionyesha Mwenyewe yeye yule jana, leo, na hata milele. Mungu, tupe ile imani halisi na aminifu, ule upendo halisi na mwaminifu, ambao utatufanya tukupende Wewe kama yule mama kulungu alivyompenda mtoto wake mchanga.

¹⁷⁵ Bwana, mbariki Bert usiku wa leo, labda hajui ninasimulia hadithi hii huku mbali sana magharibi. Ninakumbuka, Baba, nikimwona mwaka uliopita, jinsi alivyonishika na kulia, kasema, “Unamkumbuka yule kulungu, Billy?”

Nikasema, “Naam.”

Akasema, “Niliona kitu pale ambacho kilikuwa halisi. Nami nilijua ilibidi Kitu fulani kiumbe hicho, ilikuwa ni yule Mungu uliyekuwa ukinena habari zake.”

¹⁷⁶ Baba wa Mbinguni, wabariki hawa walioinua mikono yao. Umba ndani yao, Bwana, Roho wa Mungu, upendo ambao utaamini kila Neno ambalo Mungu alisema, ulio tayari kutoka nje pasipo kujali kitu kingine chochote, kile dalili inasema, kile daktari anachosema. Hatumdhili, Baba, yeye anafanya yote awezayo kufanya, lakini kama amemkatia mgonjwa tamaa, na kusema hana budi kufa, Mungu, jalia watoke nje kwa upendo mwaminifu kama huyo mama, waseme, “Niishi nife, nafsi yangu inakuonea kiu, Bwana, kama ayala aoneavyo shauku kijito cha maji.”

¹⁷⁷ Tujalie, Bwana. Wabariki. Jalia wapate shauku ya moyo wao, kwa kuwa ninawakabidhi Kwako kama kumbukumbu za Ujumbe, katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao.

¹⁷⁸ Huku tumeinamisha vichwa vyetu, kama kuna mwenye dhambi yeyote humu ndani, humu jengoni, wenye dhambi wowote, ambao kamwe hawajamkubali Yesu kama Mwokozi wao binafsi, nawe unataka kuanza vizuri, labda umesema, “Vema, siku moja nitaanza, lakini nitakapopata kuwa Mkristo, kweli nitakuwa Mkristo,” nautakia heri moyo wako mwaminifu, sasa ndio wakati wa kuanza, anza usiku wa leo. Hivi hutakuja hapa juu?

¹⁷⁹ Mwenye dhambi fulani, mvulana au msichana, mwanamume ama mwanamke, wasiomjua Yesu kama Mwokozi wao, huenda ikawa ni wafuasi wa kanisa, hilo ni sawa, ni afadhali uwe mfuasi wa kanisa na uwe mwenye dhambi, kuliko kutokuenda kanisani hata kidogo. Unafanya vizuri na yale unayofanya, lakini sasa, kwa nini usije uwe Mkristo halisi? Mbona usiweke huo upendo halisi wa Mungu moyoni mwako, unaokusukuma kwenye—kwenye wajibu wako, kusudi yule Mwalimu apate kupeleka ujumbe kwa Baba? Loo, Yeye atakutoa nje wakati fulani, Malaika atakutokea, ataweka vazi Lake la nguvu juu yako, na Yeye ata—Yeye atakupa mamlaka basi kwa kukufanya mwana mwenye mamlaka, akupe nguvu za kumfanyia kazi. Je, utakuja mbele sasa, tunapongojea kwa muda kidogo tu?

¹⁸⁰ Tunapoimba, kama ndugu atatupa sauti kidogo, sisi sote huku tumeinamisha vichwa vyetu, tukimwomba mwenye dhambi, tunapongojea:

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
Ambapo wenye dhambi wakitumbukizwa
chini ya gharika hiyo,
Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu
Iliyotolewa kutoka ninii ya Imanueli. . .

¹⁸¹ Je, utakuja mbele hapa, na kusimama hapa madhabahuni kwa muda kidogo tu, na tuombe?

. . . wenye dhambi. . .

¹⁸² “Nifanye, Bwana, Mkristo kama yule mama kulungu alivyokuwa. Alikuwa ninii halisi. . .” Mungu akubariki. Hivi hutakuja sasa pamoja na mtu huyu hapa? Mtu mmoja katika kusanyiko hili, anajitokeza, akiwa na imani kubwa.

Loo, wanapoteza madoa yao yote ya hatia;
Na wenye dhambi wakitumbukizwa. . .

Huenda ikawa ndiyo nafasi yako ya mwisho, hivi hutakuja?

. . . gharika,
Hupoteza madoa yao yote ya hatia,

Yule mwizi aliyekuwa akifa alifurahi kuona
Chemchemi hiyo katika siku yake;
Na hapo naomba mimi, ingawa ni mwovu
kama yeye,
Nioshe na kuondolea dhambi zangu zote.
Iliosha na kuondolea dhambi zangu zote,
Nioshe na kuondolea dhambi zangu zote;
Na hapo naomba, ingawa ni mwovu kama yeye,
Nioshe na kuondolea dhambi zangu zote. 🐘

60-0806 Msikieni Yeye
Eisenhower High School
Yakima, Washington Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org